

Je, Uvutaji wa sigara unafurahisha na kuchangamsha?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, lakini ni mwanzo tu na kwa muda mfupi; hii ni kwa sababu mwanzoni nikotini iliyomo katika sigara inasababisha damu kumiminika kwa wingi kupita kwenye ubongo wako. Hivyo, husababisha msisimko na kukufanya ujisikie raha. Nikotini pia inasababisha misuli mwilini kujichua na hivyo kukufanya ujisikie mchangamfu.

Baada ya muda utajisikia kinyume na ulivyojisia mwanzoni. Kama utavuta zaidi na zaidi damu na oksijeni kidogo vitatiririka mwilini na kwenye ubongo. Hii itakufanya ujisikie mchovu na mwenye huzuni.

Kwa bahati mbaya baadhi ya matangazo ya biashara au marafiki watakushawishi kwamba, uvutaji wa sigara ni safi, poa na hukufanya kujisikia mkubwa. Lakini hawaongelei madhara mabaya kiafya yatokanayo na uvutaji wa sigara na ugumu wa kuacha uvutaji huo pale utakapoizoea.

Nikotini mara nyingi huitwa kianzisho. Hii inamaanisha kwamba wakati mwingine vijana wanaanza kuvuta sigara na kisha kuhamia kwenye utumiaji wa dawa za kulevya. Hata hivyo uvutaji ni gharama.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25282>